

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA



TANGAZO

Waheshimiwa Wabunge,

Kama mnavyofahamu siku ya Alhamisi, tarehe 06 Januari, 2022 Mhe. Job Y. Ndugai, Mb. alijiuzulu nafasi ya Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Taratibu za uchaguzi wa kujaza nafasi hiyo zinaendelea.

Kwa mujibu wa Ibara ya 84 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Spika ndiye Kiongozi wa Bunge na ndiye msimamizi wa shughuli zote za Bunge. Aidha, Ibara ya 84 (8) inaelekeza kwamba Kiti cha Spika kinapokuwa wazi hakuna shughuli yoyote itakayotekelezwa katika Bunge isipokuwa uchaguzi wa Spika.

Hivyo, Kamati zilizokuwa zikutane kuanzia tarehe 10 Januari, 2022 na zilizotakiwa kukutana kuanzia tarehe 17 Januari, 2022 sasa hazitakutana kwa wakati huo na badala yake zitakutana wakati wa Mkutano wa Sita wa Bunge (1 – 11 Februari, 2022) kwa utaratibu na tarehe zitakazotangazwa.

Kwa msingi huo, mnaombwa kufika Dodoma Siku ya Jumatatu tarehe 31 Januari, 2022.

KATIBU WA BUNGE

07 Januari, 2022